JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

TAKUKURU KAGERA YAREJESHA SHAMBA LENYE UKUMBWA WA EKARI SABA KWA LIBERIUS YAMKANA

TAARIFA KWA UMMA

DESEMBA 29, 2020

1.0 Utangulizi

Ndugu wanahabari, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Kagera tumeendelea kutekeleza majukumu yetu kama yalivyoainishwa katika Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sheria namba 11 ya mwaka 2007. Katika utekelezaji wa majukumu yetu tumeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wa mapambano dhidi ya Rushwa wakiwemo waandishi wa habari, viongozi wa serkali na wananchi kwa ujumla.

Ndugu wanahabari,

TAKUKURU Mkoa wa Kagera katika utekelezaji wake wa majukumu imefanikiwa kurejesha shamba lenye ukubwa wa ekari saba(7) kwa **Liberius Yamkana** i ambaye ni mkulima na mkazi wa kitongoji cha Igabilo kijiji cha Ngararambe Kata ya Nyakaura Wilaya ya Biharamulo. Shamba hilo lenye

ukubwa wa saba (7) limerejeshwa kutoka mikononi mwa Bw.Reuben Lutonja Sahani ambaye naye ni Mkazi wakitongoji tajwa.

Ndugu wanahabari,

TAKUKURU mkoa wa Kagera mnamo tarehe 26/10/2020 tulipokea taarifa kutoka kwa **Liberius Yamkana** ambaye alikuwa akimlalamikia **Bw.Reuben Lutonja Sahani** kwa kuchukua Shamba lake lenye ukubwa wa ekari saba (7) na kuendelea kulitumia kujipatia manufaa kwa njia za hila.

Ndugu wanahabari,

Ufuatiliaji uliofanywa na TAKUKURU umeweza kubaini kuwa, **Bw. Paulo Madoshi** mnamo mwezi Agosti 2014 alikwenda kwa Bw. Reuben Lutonja Sahani ili kuazima fedha kiasi cha shilingi laki (Shs100,000/=) ili kutatua changamoto za kifamilia ambazo zilikuwa zinamkabili kwa wakati huo. Mara baada ya kumweleza **Bw. Reuben Lutonja** Sahani alikubali kumsaidia kumpatia kiasi hicho cha fedha.

Ndugu wanahabari,

Pamoja na **Bw. Reuben Lutonja Sahani** kukubali kumpatia kiasi hicho cha fedha aliweka masharti ya kupatiwa Magunia kumi na mbili ya mpuga (12) badala ya kurejeshewa kiasi hicho cha fedha. Aidha sanjari na kuweka sharti hilo pia alitaka kuwe na dhamana ya shamba lenye ukubwa wa ekari mbili. Kwa kuwa **Bw. Paulo Madoshi** hakuwa na shamba na alikuwa na changamoto za kifamilia aliweka dhamana ya shamba la shemeji yake aitwaye **Liberius Yamkana**

Ndugu wanahabari,

Ufuatiliaji wetu umeweza kubaini kuwa mara baada ya kupokea kiasi hicho cha fedha ambacho walikubaliana kulipata wakati wa mavuno **Bw. Paulo Madoshi**

katika mavuno ya mwaka 2015 ya Mpunga aliweza kurejesha magunia 4 ya mpunga ambayo kwa wakati ule yalikuwa na thamani ya shilingi elfu thelathini na tano **(Shs 35,000/=)** kila gunia ambapo magunia manne yalikuwa na thamani ya shilingi laki moja na elfu arobaini (Shs 140,000/=). Aidha pamoja na kukabidhi magunia hayo mkopeshaji ambaye ni **Bw. Reuben Lutonja Sahani** alimwambia **Bw. Paulo Madoshi** kuwa kwa kuwa ameshindwa kumpatia magunia kumi na mbili ya mpunga kwa mwaka huo kiasi cha deni kitaongezeka na akatatakiwa kulipa magunia 18 kwa msimu wa mavuno ujao.

Ndugu wanahabari,

Katika msimu wa mwaka 2016 **Bw. Paulo Madoshi** alijitahidi kuongeza juhudi katika kilimo ili aweze kulipa deni lake lakini kwa bahati mbaya hakufanikiwa kupata mpunga na kwa kuwa alikuwa amelima pia mtama walikubaliana ampatie mtana na akalipa magunia sita (6) ya Mtama ambayo kwa kipindi hicho kila gunia lilikuwa likiuzwa shilingi elfu sabini kila moja (Shs 70,000/=)kwa maana hiyi magunia sita yalikuwa na thamani ya shilingi laki nne na elfu ishirini (Shs 420,000/=). Hata hivyo mkopeshaji kwa kuwa hakuweza kupewa magunia 18 aliyodai akayaongeza tena na kumtaka amlipe magunia 36 msimu wa mwaka 2017 au amlipe fedha taslimu kiasi cha shilingi milioni mbili na laki saba.

Ndugu wanahabari,

Ufuatiliaji tulioufanya umeweza kubaini kuwa katika msimu wa mavuno wa mwaka 2017 **Bw. Paulo Madoshi** hakuweza kuvuna mpunga wa kutosha na hivyo aliweza kumpatia mdai wake kiasi cha shilingi laki tatu (Shs 300,000/=)fedha taslimu na hivyo akaendelea kudaiwa kiasi cha shilingi milioni mbili na laki nne (Shs 2,400,000/=) na kwamba **Bw. Reuben Lutonja Sahani** akampeleka mdeni wake kwa Mwenyekiti wa serikali ya Kitongoji na kumtaka amkabidhi shamba lililokuwa limewekwa kama dhamana. Hata hivyo pamoja

na kuwa dhamana ilikuwa shamba lenue ekari mbili mkopeshaji alidai kuwa dhamana imeongezeka na akashinikiza kupatiwa ekari saba na hivyo wakakubaliana nay eye akakabidhiwa ekari saba shamba ambalo ni mali ya **Liberius Yamkana** na kwamba ikaamuliwa kuwa mkoposhaji atakuwa akilitumia shamba hilo mpaka hapo atakaporejeshewa fedha zake zilizobaki.

Ndugu wanahabari,

Bw. Reuben Lutonja Sahani tangu mwaka 2017 alipokabidhiwa shamba hilo lenye ukubwa wa ekari saba amekuwa akikodisha kila ekari moja magunia manne na hivyo kila msimu amekuwa akilipwa Jumla ya magunia ishirini na nane na kwa misimu miwili yaani msimu wa 2018 na2018 tayari amejipatia magunia 56 na kwa bei ya wakati huo kila gunia lilikuwa linauzwa shilingi elfu sitini (Shs 60,000/=) hivyo ameweza kujipatia jumla ya shilingi milioni tatu laki tatu na elfu sitini (Shs 3,360,000/=)

Ndugu wanahabari

Hadi leo hii **Bw. Reuben Lutonja Sahani** kwa kukopesha kiasi cha shilingi laki moja tu tayari amekwisha jipatia kiasi cha shilingi milioni nne laki mbili na elfu ishirini pamoja na shamba lenye ukubwa wa ekari saba . Lakini wakati mtu huyu anajipatia fedha hizo **Bw. Paulo Madoshi** amekimbia na kutoroka familia yake akiwa hajuia jinsi ya kulipa deni hilo na wakati huo huo shamba la shemeji yake limechukuliwa na kusababisha taharuki katika familia

Ndugu wanahabari,

Jambo hili haliubali na ukiukaji wa sheria na mbaya zaidi huyu mkopeshaji halipii kodi mapato haya batili. Hivyo tunatoa wito kwa wananchi wote wa mkoa wa Kagera kuendelea kushirikiana na TAKUKURU na Serikali kwa ujumla katika mapambano dhidhi ya Rushwa kwani Rushwa husababisha uvunjifu wa haki za binadamu na hudhoofisha maendeleo.

Ikumbukwe kuwa tunaweza kuwa na maendeleo endelevu iwapo **HAKI** itatawala miongoni mwetu kwa kuwa **HAKI** inainua Taifa lenye watu wenye **AMANI** na **FURAHA**. Pia tumebainisha kuwa **RUSHWA** inaondoa **HAKI,** na

HAKI ikiondoka **AMANI** na **FURAHA** vitapotea. **AMANI** na **FURAHA** vikipotea hakuna **MAENDELEO** yoyote yatakayopatikana kwa Taifa na kwa mtu binafsi.

Signed
JOHN K.E JOSEPH
MKUU WA TAKUKURU (M)